Pg 2.



# Latra yatoa siku 14 mabasi kutumia tiketi mtandao halali

Na Zena Chande

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewataka wamiliki wa mabasi kutumia mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa pekee.

Ambao mabasi yao yameunganishwa kwenye mifumo isiyoidhinishwa, wamepewa siku 14 kuanzia juzi hadi Februari 15 kufanya marekebisho.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa mamlaka hiyo, Salum Pazzy alisema katika taarifa yake kuwa kuanzia Februari 15, mwaka huu yeyote ambaye basi lake halijaunganishwa kwenye mifumo iliyoidhinishwa hataruhusiwa kutoa huduma kwa kutumia mifumo isiyoidhinishwa.

"Aidha, kuanzia tarehe hiyo, utoaji na uhuishaji wa leseni za usafirishaji wa abiria utazingatia matumizi ya mifumo ya tiketi mtandao iliyoidhinishwa. Wasafirishaji wanakumbushwa kutumia wahudumu (makondakta) waliosajiliwa na Latra na wahudumu wahakikishe kila abiria ananunua tiketi ya mtandao," alisema.

Alisema hadi Januari 30, mwaka huu mifumo ya tiketi mtandao iliyokidhi vigezo vya kisheria na kuidhinishwa kuendelea kutoa huduma ni 10 huku mifumo minne ambayo haijakidhi vigezo ikizuiliwa kutoa huduma.

Alifafanua kwamba kanuni za tiketi mtandao za Latra za mwaka 2024 zinataka mifumo yote ya tiketi mtandao kujaribiwa, kuidhinishwa na mmiliki wake kupata kibali cha mamlaka ili itumike rasmi kutoa huduma kwa vyombo vya usafiri wa umma.

Alisema viongozi wa serikali wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan wamekuwa wakisisitiza azma ya serikali kuhakikisha malipo ya miamala yanafanyika kupitia mifumo ya kielektroniki.

Alisema katika hotuba ya Rais Samia ya kuaga mwaka 2025 na kuukaribisha 2026, alisema serikali inaanza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kwa kuendelea kutekeleza mkakati wa muda wa kati wa miaka mitatu 2026–2028 kwa kuongeza mapato ya serikali kupitia kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato na malipo.

"Mamlaka imeendelea kutoa elimu na kushirikiana kwa karibu na wadau wa usafirishaji ikiwemo wajengaji wa mifumo ya tiketi mtandao ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa kanuni zilizowekwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za usafiri zilizo bora, salama, zenye kuaminika na kuongeza ufanisi kwa wasafirishaji, watumia huduma (abiria) na serikali," alisema.

Alisema tangu kuanza kwa utekelezaji wa kanuni za tiketi mtandao Oktoba 2024, Latra imekaa vikao saba na watoa huduma wa mifumo hiyo kwa lengo la kuwapa elimu na kuwakumbusha matakwa ya usajili yanayotakiwa kutekelezwa ili kuruhusiwa kutoa huduma.

Alisema katika vikao hivyo, mamlaka na watoa huduma walikubaliana kuwa ifikapo Juni 30, 2025 watoa huduma wote wawe wamekamilisha matakwa yote yanayotakiwa kutekelezwa.

"Hata hivyo, hadi kufikia Desemba 30, 2025 watoa huduma watano tu kati ya 15 walikuwa wamekamilisha matakwa hayo. Desemba 30, 2025 mamlaka ilitoa taarifa ya muda wa mwisho wa kukamilisha matakwa hayo kuwa ni Januari 14, 2026 na hadi Januari 30, 2026 jumla ya mifumo 10 ya tiketi mtandao imekidhi vigezo kuendelea kutoa huduma," alisema.

Latra imetoa angalizo kwa abiria kuhakikisha wananunua tiketi mtandao wenyewe kupitia mfumo tumizi wa safari tiketi unaopatikana Play Store, App Store au kupitia anuani ya tiketi.latra.go.tz.